

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**

SHULE YA SEKONDARI BUKWE,
S.L.P 17,
TARIME.
18/12/2023

JINA LA MWANAFUNZI
S.L.P

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA NA SHULE YA
SEKONDARI BUKWE MWAKA 2024.**

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2024** katika shule ya sekondari Bukwe iliyopo Halmashauri Ya Wilaya Ya Rorya, kata ya Bukwe, kijiji cha Buganjo. Hongera na karibu sana.

Ndugu unatakiwa kuripoti shuleni ndani ya wiki tatu (3), kuanzia tarehe **08/1/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **26/1/2024**. Usipofika nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine. Aidha, kushindwa kuripoti shuleni bila taarifa yoyote ya msingi kwa tarehe tajwa hapo juu, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/ mlezi.

MAHITAJI

1. SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- I. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi.
- II. Suruali mbili zenye mzunguko wa inchi 16 kwenye tanapu, moja nyeusi na nyingine ya kijani kibichi kitambaa kizito na zenye marinda mawili. Epuka kushona au kununua suruali za piston na modal haziruhusiwi.
- III. Mkanda mweusi usiwe na kichwa kikubwa au mapambo mengine.
- IV. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi (2) visiwe vya boot na kisigino kirefu na soksi jozi mbili nyeusi.

B. WASICHANA

- I. Sketi mbili (2) ndefu mpaka kwenye kisigino, moja nyeusi na nyingine iwe kijani kibichi kitambaa kizito yenye marinda makubwa na michirizi miwili nyeupe mbele.
- II. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi.
- III. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi (2) visiwe vya boot na kisigino kirefu.
- IV. Soksi jozi mbili nyeupe.

C. KWA WOTE

- I. Sweta Moja rangi ya bluu Kwa ajili ya kujikinga na baridi.
- II. T- shirts zinapatikana shuleni.

D. NGUO ZA MICHEZO (KWA WOTE NA NI LAZIMA)

- I. Bukta rangi ya bluu na T- shirt nyeupe.
- II. Raba nyeusi

NB: Sare zote zitakaguliwa siku atakaporipoti mwanao, hivyo anapaswa kufika nazo zote zikiwa zimekamilika na zisiwe na kasoro yoyote.

2. VIFAA

- a. Daftari kubwa **09 counter book Q.2** kwa ajili ya notes za masomo yote.

- b Mkebe (Mathematical set 1)
- c. **Kamusi ya Kiingereza (English Dictionary)**
- d. Aje na **ream paper** aina ya **double A** moja (1) kwa ajili ya kufanyia mitihani ya kila mwezi.
- e. **Kalamu za wino za kutosha**
- f. Awe na **jembe moja na fyekeo moja nyumbani** kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira ya shule
- g **Aje na mche mmoja wa mti na ataupanda na kuutunza muda wore atakaokuwa shuleni** kwa ajili ya utunzaji was mazingira ya shule.
- h. **Kila mwanafunzi aje na file moja na nakala ya cheti cha kuzaliwa.**

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:-

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga/ kupigana
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kuoja/kuolewa
9. Kuapata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba.
11. Kudharau bendera Taifa.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama shuleni.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kutokuongea lugha ya kiingereza awapo shuleni.
15. Kumiliki simu,radio,kamera
16. Utoro uliokithiri bila taarifa na kutofanya majaribio na mitihani bila sababu

ZINGATIA

A Mwanafunzi awapo shuleni au mtaani anapaswa kuheshimu sheria na taratibu za shule akiwa kama mwanafunzi.

KIAPPO CHA MWANAFUNZI NA MZAZI

1. Mimi ambaye nimechaguliwa kujiunga na masomo katika shule ya sekondari Bukwe mwaka huu, ninakili kuwa nimesoma na kuelewa vyema sheria na kanuni za shule. Hivyo, ninakubali kufuata sheria na kanuni zote siku zote za uanafunzi wangu.
2. Mimi naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule, na mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na walimu kumlea mwanangu ili kuleta mabadiliko chanya katika elimu yake.

Hakikisha kuwa form ya afya imejazwa na kusainiwa na mganga wa hospital yoyote inayotambulika na kuirejesha shuleni siku atakaporipoti mwanao.

Simu namba 0767283136/0786283136 – MKUU WA SHULE.

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

RORYA DISTRICT COUNCIL

BUKWE SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

Full name

Age Height (in Cms) Weight

1. Blood count (Red and white).....

2. Stool examination

3. Urinalysis.....

4. Syphilis and other V.D

5. T.B and leapers Test

6. Eye Test

7. Ear Test

8. Chest Test

9. Adnominal Test

10. Plano Test (girls)

11. Spleen

Addition information e.g physical defects or impairments, infection chronic or family Diseases (e.g sickle – cell) Inability to eat certain food e.t.c.

.....
.....
.....
.....

I certify that above named students is fit/ is not fit to pursue secondary education

Date

Signature

Date

Station

.....

Official stamp